**East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature**
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-8 | Issue-9 | Sep- 2025 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2025.v08i09.009

OPEN ACCESS

**Original Research Article**

# Uchambuzi wa Ujumi katika Muziki wa Benga wa Jamii ya Wakamba: Mkabala wa Umtindo

Carolyne Muthini Mutuku[1*], Dkt. John Khaisie Wanyama[1], Dkt. Timothy Kinoti M'ngaruthi[1]
[1]Idara ya Masomo ya Jamii, Chuo Kikuu cha Embu, S. L. P. 6-60100, Embu, Kenya

**Article History**
**Received:** 18.07.2025
**Accepted:** 15.09.2025
**Published**: 18.09.2025

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Muziki wa Benga ni utanzu maarufu nchini Kenya. Hujitambulisha kwa sifa ya mdundo na mapigo ya kasi pamoja na ustadi wa msanii wa kucheza gitaa na kuimba kwa mtindo maalum. Licha ya ustadi wa matumizi ya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, bado kuna pengo la kitaaluma kuhusiana na uchanganuzi wa kina wa jinsi vipengele vya mtindo katika muziki huu vinavyotumika kuimarisha ujumi. Utafiti huu ulilenga kuchanganua namna mikakati ya mtindo inayotumika katika muziki huu inavyoimarisha ujumi na athari za kijamii. Uchunguzi huu uliongozwa na kielelezo cha nadharia ya Umtindo. Umtindo hufasiri na kuhakiki tungo kwa kuzingatia mtazamo wa kiisimu kama taaluma iliyo na uhusiano wa karibu na fasihi. Uchunguzi wa kimtindo huhusisha namna lugha inavyotumika katika matini ili kujenga maana na athari. Usampulishaji ulifanywa kimakusudi ambapo nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ziliteuliwa. Ukusanyaji wa data ulihusisha upakuaji wa nyimbo za Benga kutoka kwa mtandao wa kijamii wa *Youtube* na unakili wa mishororo yake. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumika kubainisha mikakati ya kimtindo na kuchanganuliwa kimaelezo kwa kuelekezwa na mihimili ya nadharia ya umtindo. Data zilikuwa ni maneno, dhana, kauli, virai na sentensi zinazotumiwa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba zinazohusisha vipengele vya kimtindo. Utafiti uliweza kubaini kuwa waimbaji hao hutumia vipengele vya kimtindo kuimarisha ujumi wa kihalisia, kigothiki, kimapenzi, kisiasa, kitamaduni na ujumi wa kiishara. Utafiti huu unasisitiza uhusiano thabiti baina ya muziki, utamaduni na lugha katika jamii, ukionyesha dhima ya ujumi katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Utafiti huu ni muhimu katika kuufanya muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kutambulika katika nyanja za utafiti wa kielimu wa fasihi na lugha kama kategoria ya nyimbo za kitamaduni. Utachangia taaluma ya isimu na mawasiliano.

**Keywords:** Ujumi, Mtindo, Muziki, Benga, Wakamba, Mikakati.

**Copyright © 2025 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Muziki ni njia mojawapo ambayo wanajamii hutumia kuwasiliana kuhusu masuala tofauti kama vile mapenzi, siasa, kifo na dini. Baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na muziki ni kama vile; kupanua ujuzi wa kijamii, kukuza ushirikiano katika jamii, kukuza ubunifu na kuwasilisha hisia za wanajamii. (Okal, 2020). Mawasiliano ya kimuziki hutofautiana katika jamii mbalimbali kwani mitindo wanayotumia wasanii mbalimbali hutegemea mahali wanapoishi, kiwango cha elimu, tofauti za kitamaduni na vyeo vyao kijamii (Butler, 2004).

Muziki wa Benga ni aina ya muziki ambao huwasilishwa na waimbaji, wachezaji pamoja na ala za muziki kama vile gitaa na ngoma. Doyle (2017) anarejelea aina hii ya muziki kama 'thieta ya muziki.' Hii ni kwa sababu hujikita katika umbo la kimuundo linalohusisha kuimba, kuchezesha viungo vya mwili na dayolojia ili kueleza jambo kama linavyotokea katika maisha ya kila siku ya binadamu. Ploti katika muziki wa Benga huundwa kwa mwanzo, kati na mwisho (Doyle, 2017). Muziki wa Benga ni utanzu maarufu nchini Kenya na hujitambulisha kwa sifa ya mdundo na mapigo ya kasi pamoja na ustadi wa msanii wa kucheza gitaa kwa namna maalum (Red Bull Music Academy, 2019). Kulingana na Muema (2019), muziki wa Benga nchini Kenya umegawanyika kulingana na maeneo. Kuna Benga ya Magharibi, ya Kati na Mashariki. Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unapatikana katika eneo la Mashariki. Muziki huu umekuwepo tangu miaka ya sitini ambapo kulikuwepo na waimbaji maarufu kama vile,

***Corresponding Author:** Carolyne Muthini Mutuku
Idara ya Masomo ya Jamii, Chuo Kikuu cha Embu, S. L. P. 6-60100, Embu, Kenya

Kakai Kilonzo, Peter Muambi na Bosco Mulwa. Kufikia sasa, idadi ya waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba imeongezeka (Muema, 2019). Waimbaji wa kisasa katika jamii ya Wakamba ni kama vile Alphose Kioko, Alex Kasau na Ben Mbatha. Muziki wa waimbaji hawa huchezwa kila siku katika vipindi vya redio, runinga na mitandao ya kijamii kama vile *Youtube* (Kithome, 2012).

Kwa mujibu wa Anudo na Awuor (2018), uwasilishaji wa maudhui katika muziki huweza kufichwa kwa kutumia mitindo mbalimbali ya utunzi. Kusudi la kutumia mitindo fiche ni kuifanya hadhira kufikiria zaidi ndiposa iweze kutambua maana inayopitishwa. Dhana ya mtindo haiwezi kutokea katika ombwe tupu bali hupata maana lugha inapotumika kuwasilisha ujumbe. Wasanii hutumia mtindo katika tungo zao hasa mashairi na nyimbo kwa kusudi la kupata athari za kiujumi (Leech, 1969). Kwa mujibu wa Timu ya Historia ya Kenya (2025), mvuto katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba husababishwa na matumizi ya mikakati ya kipekee ya mtindo. Hii ni pamoja na mapigo ya gitaa yenye mdundo maalum na mchanganyiko wa lugha ya asili na maudhui kwa jumla. Vipengele vya mikakati ya kimtindo hutumika kama chombo cha kusimulia hadithi, kuhifadhi utamaduni na masuala ya kijamii (Muema, 2019).

Uchunguzi wa ujumi wa kisanaa katika muziki huhusisha uchambuzi wa jinsi vipengele vya kisanaa vilivyo ndani ya tungo za muziki vinavyochochea hisia, kufikisha maana za kitamaduni na kuunda mtazamo wa hadhira. Watafiti wengi wameeleza kuwa sifa za kiujumi kama vile wizani, melodi, mdundo na lugha ya kishairi si mapambo tu, bali ni nguzo kuu zinazotoa nguvu ya mawasiliano katika nyimbo (Leech, 1969; Scruton, 1997*)*. Kwa mujibu wa Tagg (2012), ujumi katika muziki hufanya kazi kama jambo la kawaida na la utamaduni mahususi, ambapo wasikilizaji hufasiri kazi za muziki kupitia ishara na mitindo inayotambulika kijamii. Waimbaji huweza kutumia maneno sahili yanayoambatana na ishara za lugha ambazo ni rahisi kueleweka na hadhira lengwa. Lengo kuu la kutumia maneno sahili na ishara za lugha likiwa ni kuivutia hadhira lengwa (Afipah na wenzake 2022). Kwa mujibu wa Bitabaje (2017) baadhi ya sababu zinazofanya wasikilizaji wa nyimbo kuvutiwa kusikiliza nyimbo ni haiba ya mwimbaji pamoja na maudhui yanayowasilishwa.

Uzuri au ujumi hutambulika kwa namna tofauti katika jamii mbalimbali. Kwa mfano katika baadhi ya jamii uzuri hujengwa kupitia sifa za mwonekano wa kimwili kama umbo au rangi ya ngozi, ilhali katika jamii nyingine uzuri huweza kuhusishwa na maadili mema, ujuzi wa sanaa au kipaji cha muziki. Pia, kuna jamii zinazotambua uzuri kupitia mavazi ya kitamaduni na mapambo ya kifani, wakati zingine huelekeza uzuri katika nafasi na heshima ya kijamii anayoshikilia mtu. Aidha, ilibainika kuwa matumizi ya vipengele vya kiujumi katika fani na maudhui ya nyimbo huchangia kuburudisha, kuelimisha, kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii na kuutambulisha utamaduni wa jamii husika (Laswai, 2015).

Mutisya na Muhoro (2022) walichunguza thamani ya ujumi na utendaji katika nyimbo za michezo za watoto wa jamii ya Wakamba. Walibaini kuwa nyimbo hizi zimejikita kwa kina katika tamaduni za jamii ya Wakamba na hutumika kama vyombo vya kuwasilisha thamani muhimu za ujumi wa kisanaa. Hasa, nyimbo hizo zinasisitiza thamani za ujumi wa masuala halisi kama vile; urafiki na umoja, uwajibikaji, ufahamu wa masuala ya mazingira, uhusiano wa ukoo, tamaduni na thamani ya bidii kazini na kukwepa uvivu. Utafiti wao unaonyesha jinsi ujumi unavyoimarishwa katika nyimbo hususan za watoto wa jamii ya Wakamba. Hata hivyo, mtazamo wao umesalia katika nyimbo za michezo ya watoto pekee na haujapanuliwa kujumuisha aina nyingine za muziki wa kisasa kama vile muziki wa Benga, ambao umeibuka kama njia yenye ushawishi mkubwa wa uelezaji wa kitamaduni miongoni mwa jamii ya Wakamba.

Licha ya ustadi wa matumizi ya mtindo katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, bado kuna pengo la kitaaluma kuhusiana na uchanganuzi wa kina wa jinsi vipengele vya mtindo katika muziki huu hutumika kuimarisha ujumi. Tafiti nyingine zimejikita katika maudhui na vipengele vya utendaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba, huku uchunguzi wa kina wa vipengele mahsusi vya mtindo ukipuuzwa. Jambo hili linaacha pengo katika kuelewa jinsi chaguzi za kimtindo zinazofanywa na waimbaji wa Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba huchangia katika mvuto na utamaduni wa jamii hii. Hivyo basi, kuna pengo la kitaaluma katika kuelewa jinsi wasanii wa Benga wa jamii ya Wakamba wanavyotumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi katika nyimbo zao. Utafiti huu ulijishughulisha na kuziba pengo hili.

## 2.0 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umtindo kama ilivyofafanuliwa na Geoffrey Neil Leech (1969). Nadharia hii hufasiri na kuhakiki tungo katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma iliyo na uhusiano wa karibu na fasihi. Vile vile nadharia hii hueleza namna mtu katika jamii anavyotumia lugha katika muktadha fulani na kwa lengo maalum. Kulingana na Leech (1969) umtindo hufungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu katika kufasiri tungo. Anasema kuwa mbinu za lugha kama vile jazanda, sitiari, usambamba, tashbihi na kinaya haziwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana ya kiisimu. Kwa hivyo umtindo ni uwanja ambamo masuala ya lugha hushughulikiwa kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu. Leech anaiona nadharia ya umtindo kama nadharia iliyoko kati ya fasihi na isimu. Hii ina maana kuwa matumizi ya vipengele vya kiisimu hayawezi kupuuzwa tunapohakiki mtindo katika mkabala wa kifasihi.

**2.1 Mihimili ya Nadharia ya Umtindo**

Nadharia ya umtindo ina viwango mbali mbali vinavyoweza kuchunguzwa kwa mujibu wa Leech na Short (1981). Viwango hivyo ni kama vifuatavyo:

- Kiwango cha udhihirishaji; kiwango hiki kinahusu jinsi maumbo ya lugha yanavyotamkwa(fonolojia) na kuandikwa (grafolojia). Kiwango hiki hujihusisha na uchunguzi wa mtaala wa sauti za lugha fulani pamoja na kanuni zinazotawala utamkaji wa sauti za lugha hiyo. Mfano wa vipengele vya kifonolojia ni kama vile; uradidi, urudiaji wa vokali na konsonanti.
- Kiwango cha Umbo; hiki ni kiwango kinachohusisha uteuzi wa msamiati na maneno maalum. Ni kiwango cha sajili au kiwango cha kimsamiati (leksia). Leksimu kwa kawaida hurejelea maneno katika lugha fulani. Leksia ni kiwango cha kimtindo ambacho kinajihusisha na maneno, istilahi na dhana za lugha fulani.
- Kiwango cha Sintaksia na Mofolojia; Kiwango hiki hujishughulisha na vipengele vya kimtindo vinavyojitokeza kwenye sentensi. Hiki ni kiwango kinachojihusisha na sintaksia pamoja na mofolojia. Kwa kawaida watu huzungumza kwa kutumia sentensi wala si kwa maneno pweke. Lengo la kiwango hiki ni kuchanganua muundo wa ndani wa sentensi katika lugha na umuhimu wa sentensi hizo zinapopangiliwa kwa mpangilio maalum (usambamba), matumizi ya nomino na vitenzi kwenye sentensi hizo, dhana, maneno na istilahi zinazotumika.
- Kiwango cha Kisemantiki; kiwango hiki kinajihusisha na maana ya maneno na sentensi za lugha fulani. Kinahusu miundo ya lugha na lugha ya kitamathali. Ni namna lugha inayotumiwa inavyoathiri maana katika kazi za fasihi. Kinahusisha matumizi ya maneno na jinsi maana za maneno hayo zinavyofasiriwa katika hali za kawaida.

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa kimaelezo ulitumika kuchanganua na kuwasilisha data za utafiti huu. Kulingana na Kothari (2017) muundo wa utafiti wa kimaelezo huhusisha kuchunguza jambo katika hali yake halisi. Utafiti wa kimaelezo hutambua na kueleza sifa za jambo fulani kama vile mtu, kikundi au jamii. Muundo huu wa utafiti huchunguza hali halisi ya kitu na kueleza miundo ya jamii pamoja na hafla au miktadha ya kijamii.

Walengwa katika utafiti huu walikuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba waliotunga kwa kuzingatia vipengele vya kimtindo. Sampuli ziliteuliwa kimakusudi kutoka kwa nyimbo za mziki wa Benga wa jamii ya Wakamba. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usampulisjaji wa kimakusudi huchunguza na kuchuja data ili kupata sampuli iliyo na sifa zinazohitajika. Katika usampulishaji wa kimakusudi, uteuzi wa data hufanywa kwa kuegemea maamuzi ya kibinafsi kwa minajili ya uelewa wa kina wa kianachotafitiwa.

Data za utafiti huu zilikuwa ni maneno, dhana, kauli, virai na sentensi zinazotumiwa na waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba ambazo zilikuwa vipengele vya kimtindo. Enon (1998) anasema kuwa mkabala wa kithamano ni mkabala usio wa kiidadi. Ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Uchambuzi wa kimaelezo unategemea zaidi ustadi wa mtafiti na ufahamu wa kibinafsi wa mkutadha wa kijamii ambapo data hukusanywa. Mkazo katika utafiti wa aina hii unatiliwa katika kuelewa jambo badala ya kulitabiri au kulieleza. Mtafiti alisikiliza nyimbo za muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba na kuteuwa nyimbo saba zilitungwa kwa kuzingatia mikakati ya kimtindo. Nyimbo za muziki zilizoteuliwa ni: *Wakatimba Kumbavu (WK)*- Wakatimba Pumbavu wake Ken Maria, *Sikala Yakwa (SY)* -Sigara Yangu wake Ben Mbatha, *Germany by Foot* (GF*)*- Ujerumani kwa Miguu wake Ken Maria, *Munene ko Woolilwe?* (MK)- Mkubwa kwani Ulisahau? wake Ken Maria, Raha Ndukauna (RN)- Raha Haisaidii wake Bosco Mulwa, *Wasa Mbili* (WM)- Rafiki Kupe wake Alex Kasau na Sio Mageni (SM) wake Anita Mwiitu wa Kitunguu. Mtafiti alizisimba nyimbo zilizoteuliwa kwa kutumia alama za kwanza za mada za nyimbo hizo ili kufanikisha uelezaji. Maadili yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data kwa kuhakisha kuwa data zilizokusanywa zilitumika tu kuafikia madhumuni ya utafiti huu pekee. Pia, mtafiti alituma ombi na kupata kibali cha kukusanya data kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi, nambari ya leseni NACOSTI/P/24/39217.

## 4.0 UJUMI KATIKA MUZIKI WA BENGA WA JAMII YA WAKAMBA

Kwa mujibu wa Ponera (2014), ujumi ni neno lililotafsiriwa kutoka kwa neno la Kiingereza “aesthetics.” Neno hili lilitumika kwa mara ya kwanza na Alexander Gottlieb Baumgarten mwaka wa 1735. Ujumi ni tawi la falsafa ambalo hushughulikia ubaya, uzuri, ladha, uhasi, ubora au urembo. Katika muktadha wa muziki, ujumi husaidia kuelewa namna vipengele vya sauti, mitindo ya uimbaji na mpangilio wa tungo vinavyochangia urembo na maana ya muziki. Kant (2000) anaeleza kuwa ujumi ni taaluma inayochunguza maamuzi ya ladha, ambayo huwa ya mtu binafsi lakini yanaweza kueleweka au kukubalika na watu wote. Alidokeza kwamba tunapohukumu kitu kuwa kizuri, tunakifurahia bila kutegemea faida yoyote binafsi, tunapendezwa na uzuri wake tu, si kwa sababu kina manufaa au kinaendana na maadili. Thiong’o (1986) alisisitiza kuwa ujumi wa Kiafrika ni wa kiutendaji na wa kijamii unaotegemea sanaa simulizi na huambatana na maana za kimaadili, kiroho na kisiasa.

Leech (1969) anadokeza kuwa mawasiliano ya kiujumi ni mchakato ambao kazi ya sanaa huwasilisha maana ya kina kuliko ile ya mawasiliano ya kawaida.

Mchakato huu wa kiujumi mara nyingi husababisha hisia na uelewekaji wa kazi ya sanaa kwa njia inayozidi mbinu za mawasiliano ya kawaida. Kwa mujibu wa Leech, ujumi sio tu kuhusu umbo au uzuri; unahusisha mwingiliano wa kina kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira. Leech aliamini kuwa ujumi una uwezo wa kipekee wa kuwasilisha mawazo na hisia tata, ambazo huenda zisiweze kuelezeka kwa lugha ya kawaida. Nadharia ya umtindo inasisitiza mwingiliano kati ya msanii na hadhira, ikieleza kwamba thamani ya sanaa au ujumi imo katika uwezo wake wa kuwasilisha maana na kuamsha hisia za hadhira.Waimbaji wa Muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wametumia mikakati ya kimtindo kuimarisha ujumi katika miziki yao kama ifuatavyo:

**4.1 Ujumi wa Kihalisia**

Ujumi wa kihalisia hurejelea mbinu za kisanaa zinazolenga kuonyesha maisha kama yalivyo, kwa kuzingatia uzoefu wa kila siku pamoja na hali halisi za kijamii na kibinadamu, bila kupotosha ukweli wala kutilia chumvi. Katika muktadha wa muziki, ujumi wa kihalisia hutumika kuonyesha hisia za kweli, kuangazia changamoto za maisha halisi na kuunda uhusiano wa karibu baina ya mwimbaji na wasikilizaji kwa kuakisi hali zao halisi. Kwa mujibu wa Eagleton (1990), uhalisia katika sanaa hulenga kuzalisha upya hali halisi ya uzoefu wa kawaida na kuufanya uwe na ukweli unaotambulika. Jambo hili huongeza uwezo wa kazi kueleweka kirahisi na kugusa hisia za hadhira. Ujumi wa kihalisia unajitokeza katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo;

Katika muziki SY katika ubeti ufuatao;
*Ni kwithiwa ni murasta, na niishia kimrasta* - Kwa maana mimi ni mrasta, na huwa ninaishi kama mrasta
*Nikyongaa ta murasta, ngakusya vangi ta murasta* - Huwa natafuna miraa kama mrasta, na kuvuta bangi kama mrasta
*Sikala yakwa ni ro*sta*, inyusawa ni mura*sta - Sigara yangu ni rosta, huwa inavutwa na mrasta (ubeti wa saba)

Katika ubeti huu ujumi wa kihalisia unajitokeza kupitia mtindo wa urari anaotumia mwimbaji. Kwanza, mwimbaji anaeleza maisha ya mtu wa kundi la "rasta" kwa kutumia lugha rahisi, ya moja kwa moja na inayojikita katika shughuli halisi kama vile kuishi, kutafuna miraa, kuvuta bangi na sigara. Hizi ni tabia na mitindo ya maisha inayotambulika na baadhi ya watu katika jamii, hivyo zinaakisi maisha ya kila siku bila mapambo wala kuficha uhalisia wa hali hizo. Kwa mujibu wa kanuni za ujumi wa uhalisia, kazi ya sanaa inapaswa kuonyesha hali halisi za jamii, wahusika wa ukweli na mazingira yanayofanana na yale ambayo wasikilizaji hukumbana nayo (Eagleton, 2008). Ubeti huu unatimiza hilo kwa kuonyesha wazi mtindo wa maisha ya mtu wa kundi la kijamii "rasta," na hivyo kuwawezesha wasikilizaji kuhusisha ujumbe huo na maisha halisi yanayowazunguka. Zaidi ya hayo, matumizi ya urari kama vile, urudiaji wa muundo wa kisarufi: "ni murasta… kimrasta… ta murasta... ni rosta… ni murasta," unatoa muundo wa ruwaza zinazoiga mzunguko wa maisha ya kila siku. Hili linaendana na maelezo ya Leech (1969) kwamba urari huweza kutumika kuonyesha mwendelezo wa maisha na kuongeza uhalisia kupitia mtiririko wa kisauti.

Pia ujumi wa kihalisia unajitokeza katika muziki SM kama ifutavyo:
*Kwakwa syo mbesa ti kindu, indi akaunti ni mbinge-* Kwangu pesa si kitu, lakini akaunti zimefungwa
*No nguutumia kindu kasweetie naku mbumiisye* - Nitakutumia kitu kidogo mpenzi nivumilie (ubeti wa nne mshororo wa kwanza na wa pili)

Kauli hizi zinabainisha changamoto halisi za kifedha ambazo watu wa mjini hukumbana nazo. Msanii anatumia hali ya akaunti zilizofungwa kuonyesha matatizo ya kiuchumi kwa namna ya uhalisia unaoeleweka kwa hadhira.

> *Nikwoona TikTok nyie kana ngeeewa muleelo, na yuyu niende tuvange wikendi imwe tukomane-Huwa nakuona TikTok mtoto, naishiwa nguvu, na sasa nataka tupange wikendi moja tuonane*

*Maneno haya sio mageni mjini, nikwatya nimukuelewa kina ngwasya, maneno haya sio mageni mjini tauni kuyingwa ndia andu yu nakyanuku-* Maneno haya sio mageni mjini, nina uhakika mnaelewa ninachokisema, maneno haya sio mageni mjini, mjini hakuna mjinga watu sasa wamechanuka.(ubeti wa tano)

Katika ubeti huu, mwimbaji anatumia mifumo halisi ya mahusiano ya kisasa, ikiwemo mitandao ya kijamii 'TikTok', kuonyesha mapenzi ya mjini. Huu ni ujumi wa kihalisia unaojikita katika maisha ya kila siku ya vijana wanaishi mjini. Urudiaji wa kibwagizo *"maneno haya sio mageni mjini… mjini hakuna mjinga, watu sasa wamechanuka"* unajenga taswira ya jamii ambayo imeelimika na haiwezi kudanganywa. Hii ni kauli ya hekima ya kijamii inayotokana na hali halisi ya maisha ya mjini, ambapo watu wamepata ujuzi kutokana na uzoefu wa maisha.
Vilevile katika muziki RN ubeti huu;
*Raha ndukauna kuma tene ndukauna* - Raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii
*Tindikana nawo indi mwiso ukaiya* -Sukumana nayo lakini mwisho utalia
*Maisha me muyo ta woona mbesa winasyo* - Maisha ni tamu, kwanza ukiwa na pesa
*Indi nitheelaa ukakopa mbaka sya uya* - Lakini huwa zinaisha unakopa hadi za chakula
*Starehe sya aka na kuteewa syi muyo* - Starehe za wanawake na kuuziwa zina ladha
*Musaala waku wiminiwa baa ni aka-* Mshahara wako utamalizika kwenye klabu kwa wanawake
*Na wathelelwa mayosa abiria ungi-* Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine,

*Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini,

*Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu (uvundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki*- Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu (jifunze kudhibiti pesa zako kijana na uachae kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa sio rahisi kuzipata) (ubeti wa kwanza)

Ubeti huu unaakisi ujumi wa kihalisia kupitia uwasilishaji wa maisha halisi ya kijamii kwa kutumia lugha ya moja kwa moja, maudhui ya kila siku na hisia za kweli zinazotokana na hali za maisha. Katika ubeti huu, mwimbaji anazungumzia matatizo yanayotokana na maisha ya starehe kama vile matumizi mabaya ya pesa, anasa, ulevi, mahusiano ya kimapenzi ya muda mfupi na hali ya umaskini unaofuata. Lugha inayotumika ni ya kawaida, ikiwakilisha kwa uaminifu hali ambazo wasikilizaji wengi wanaweza kuzitambua au kuhusiana nazo. Matumizi ya kauli "*ukakop*a *mbaka sya uya-* unakopa hadi za chakula" na "*uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya*- unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini" zinawasilisha uhalisia wa matatizo ya kiuchumi na kijamii yanayowakumba watu wa kawaida.

Vilevile, kibwagizo cha kejeli "fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu" kinawasilisha ujumbe wa tahadhari kwa njia ya kuchekesha lakini yenye uzito, hivyo kuchanganya uhalisia na mbinu za kisanaa. Ingawa kibwagizo hicho kinaweza kuonekana kama mchezo wa lugha kwa mtazamo wa ujumi wa kisasa, bado kinaendeleza dhamira ya ujumi wa kihalisia kwa kusisitiza umuhimu wa matumizi bora ya rasilimali, jambo ambalo ni sehemu ya maisha ya kila siku. Kwa mujibu wa Leech (1969) na Menninghaus na wenzake (2022), mikakati ya kimtindo huimarisha maana ya ujumbe huku ikitoa mvuto wa kisanaa unaobeba hisia za muktadha halisi wa kijamii. Hivyo basi, ubeti huu ni mfano bora wa matumizi ya ujumi wa kihalisia katika muziki wa Kiafrika wa kisasa kwa kuonyesha changamoto za kijamii kupitia lugha ya wazi na taswira halisi za maisha.

**4.2 Ujumi wa Kigothiki**

Kwa mujibu wa Byron & Townshend (2014) neno gothiki linarejelea mtindo au aina ya kazi ya sanaa inayohusisha vipengele vya giza, mafumbo, hofu na mambo ya ajabu yasiyo ya kawaida. Istilahi hii hutumika katika fasihi na sanaa kuonyesha mazingira ya kutisha, hisia kali kupita kiasi na maudhui ya ajabu kama vile mizimu na kifo. Vipengele vya kigothiki mara nyingi hutumika kuchunguza matamanio yaliyofichwa, wasiwasi wa kijamii, au mmomonyoko wa maadili, hivyo kuviwezesha kuwa nyenzo zenye nguvu katika kuwasilisha maana ya kimafumbo na kina cha kisaikolojia katika fasihi (Byron na Townshend, 2014). Katika utafiti huu ujumi wa kigothiki umeimarishwa ifuatavyo;

Kwa mfano, kibwagizo cha beti za muziki RN;
*Ndwike masavu, ika masavu, eka uvitya masavu* - Fanya hesabu, fanya hesabu, wacha kukosea hesabu.

Kurudiwa kwa onyo hili kunawasilisha hisia nzito za kijamii. Jamii inaonywa dhidi ya ubadhirifu wa pesa na kuzingatia matumizi mwafaka. Mtindo huu unaibua ujumi wa kigothiki kwa kuunda mazingira ya hofu, tahadhari na hali ya hatari inayotokana na uharibifu wa maadili na kuporomoka kwa utu wa binadamu ndani ya maisha ya kila siku ya kukosa fedha au kushindwa kiuchumi. Kwa mujibu wa Bradley (2018), ujumi wa kigothiki hujitokeza pale ambapo hali ya kawaida ya maisha huonyeshwa ikidorora kuelekea maangamizi ya kiakili au kijamii, jambo linaloonekana wazi katika kibwagizo hiki. Onyo hili halihusu tu udhibiti wa fedha, bali pia linaashiria hatari ya mtu kupoteza mwelekeo wa kimaadili na kijamii. Kwa hivyo, inajenga muktadha wa kihisia unaoendana na mvutano kati ya udhibiti wa mantiki na kuporomoka kwa hali ya kawaida, mojawapo ya viini vya ujumi wa kigothiki kwa mujibu wa (Spooner, 2007).

Vilevile katika muziki SM ubeti ufuatao:
*Ve syindu ngwatie kwona Anita ngavewa kyeva*- Kuna mambo ninayoyaona , Anita kweli nahisi huruma,
*Nayuyu mbangie niwete, ula ukumena amene yu*- Na sasa nimeamua kuyasema, atakaye nichukia anichukie

*Maneno haya sio mageni mjini, nikwatya nimukuelewa kila ngwasya, maneno haya sio mageni mjini tauni kuyingwa ndia andu yu nakyanuku*.-Maneno haya sio mageni mjini, nina uhakika mnaelewa ninachokisema, maneno haya sio mageni mjini, mjini hakuna mjinga watu sasa wamechanuka.(ubeti wa kwanza)

Ubeti huu unaonyesha wasiwasi na msukumo wa kihisia. Kauli "kuna mambo ninayoyaona, Anita kweli nahisi huruma, na sasa nimeamua kuyasema, atakaye nichukia na anichukie" inaomnyesha hisia kali za kusikitisha zinzzomsukuma mwimbaji. Wasiwasi wa mambo kutendewa visivyo na msongo wa ndani ni dhihirisho la kigothiki, ambapo nafsi hujipata ikikabiliwa na mapambano ya ndani, hofu ya upweke na hukumu ya jamii.

Uradidi wa kibagizo cha beti za muziki huu (SM) "*maneno haya sio mageni mjini..."* umetumika kama kiashiria cha mafumbo ya kijamii. Marudio haya yanabeba uzito wa kifasihi wa kigothiki: yanafanya muziki uwe na sauti ya kinabii inayotoa onyo kuhusu hali ya jamii, kwa namna ya fumbo linalotisha.

Pia katika muziki SM beti zifuatazo:
*Nienda twose kalumu kasweetie naku tutundume, no tukome utuku muima mbevi ndakwitya*- Nataka tuchukue chumba, mpenzi tuzungumze, tunaweza kulala usiku mzima (ubeti wa tano, mshororo wa kwanza na wa pili)
*Nikwoona TikTok nyie kana ngakwatwa ni muleleo*- huwa nakuona TikTok mtoto naishiwa nguvu

*Na yuyu niende tuvange wikendi imwe tukomane* – Na sasa nataka tupange wikendi moja tupatane (ubeti wa sita mshororo wa kwanza na wa pili)

Kauli kama *"Nataka tuchukue chumba, mpenzi tuzungumze, tunaweza kulala usiku mzima"* au *"Huwa nakuona TikTok mtoto, naishiwa nguvu"* zinaibua matamanio ya mwili na mapenzi yaliyofichwa. Katika mtazamo wa kigothiki, matamanio haya yanaweza kuonekana kama nguvu za giza zinazoweza kupelekea mmomonyoko wa maadili au hofu ya jamii kuhusu mabadiliko ya mienendo ya vijana.

Ujumi wa kigothiki pia unajitokeza katika muziki WK, Katika ubeti huu;
*Wakatimba nyie kweli nguseng'a ni tabia syaku* - Wakatimba mimi kweli nashangaa kwa tabia zako
*Ona kutwika wi mwanake wi akili ndogo* - Hata ingawa wewe ni mrembo una akili ndogo
*Muvaile waku ni ukengana wi mundu wa vata* - Mavazi yako yanaweza kudanganya kuwa wewe ni mtu wa maana
*Indi malondu maku we ve amwe me kithekani* - Lakini bado wapo kondoo wako walio kichakani
*Niona wi ndia Wakatimba wi mana* - Naona ukiwa mjinga Wakatimba wewe ni bure
*Na ndinakuuma Wakatimba kumbavu* - Na sijakutusi Wakatimba mpumbavu (ubeti wa kwanza)

Urudiaji wa maneno kama "*kumbavu* – mpumbavu" pamoja na kauli za kudhalilisha kama "*niona wi ndia* - naona ukiwa mjinga" zinaonyesha namna lugha inavyotumika kama chombo cha kutoa hukumu kali na kuibua muktadha wa maumivu ya kihisia. Maneno haya, ingawa si ya kitafsida, yana mvuto wa kimakabiliano kwa kuwa yanatoka nje ya mawasiliano ya kawaida na yanahusisha mashambulizi ya moja kwa moja dhidi ya utu wa mhusika. Kwa mujibu wa Bradley (2018), vipengele vya kigothiki hujengwa kupitia hisia za uwoga na hali ya kuvunjika kwa maadili, ambavyo vyote vinaonekana bayana katika ubeti huu. Lugha isiyo ya kitafsida inayotumika hapa haitumiki tu kwa lengo la kukemea, bali pia inawasilisha hali ya kihisia iliyochafuka ambayo inaweza kuibua huzuni au mshtuko kwa upande wa msikilizaji. Kwa njia hii, ujumi wa kigothiki huchangia kuongeza mvuto wa kazi ya sanaa kwa kuimarisha kina cha kisaikolojia na dhamira ya kuhoji maadili na tabia za kijamii. Kwa hivyo, aina hii ya ujumi huibua tafakari za kina kuhusu hali ya maisha ya binadamu na jamii inayomzunguka.

**4.3 Ujumi wa Kimapenzi**

Ujumi wa kimapenzi ni mtindo wa kisanaa unaolenga kuonyesha hisia za ndani za mtu, uzoefu wa kibinafsi, ubunifu wa fikra na uzuri wa mazingira ya asili au mambo ya kushangaza yenye mvuto. Mtindo huu hujitokeza kama njia ya kupinga sanaa za zamani zilizozingatia mantiki na kanuni zisizobadilika (Berlin, 1999). Katika muziki, ujumi huu huonekana wazi kupitia mbinu za kisanaa kama vile kutumia maneno yenye hisia kali, kueleza mapenzi au uchungu wa moyo, kutumia taswira za uzuri wa kiasili na kurudia maneno ili kusisitiza hisia. Ujumi wa kimapenzi huweza kujidhihirisha kupitia miundo mirefu ya sentensi iliyojaa hisia, ikionyesha ubinafsi wa hali ya juu na maonyesho ya kina ya uzuri (Abrams, 1999; Fitzgerald, 2010). Hili linajitokeza katika muziki RN ambapo mwimbaji anatumia sentensi tongole ifuatayo;

> *Woona wesa uvitya masavu ukatheelawa kitimba ni syana wakua ukomete valanda wa nyumba, nundu waiye mbesa ta ngaange* - Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada mwa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa (ubeti wa nne mshororo wa sita)

Katika sentensi hii ujumi wa kimapenzi unaibuka kupitia matumizi ya sentensi ndefu iliyojaa hisia, ambayo ni kiashiria muhimu cha mtindo huu wa ujumi kama inavyobainishwa na (Abrams, 1999; Fitzgerald 2010). Kupitia sentensi kama:

"Utakapokosea hesabu utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada wa nyumba, kwa sababu ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa..."(mshororo wa sita ubeti wa kwanza)

Katika dondoo hili, mwimbaji anajenga picha ya adhabu na fedheha anayoweza kupata mtu anayekosea katika maisha yake. Kauli *"utapigwa mateke kiunoni na watoto ukizeeka ukiwa umelala ferada mwa nyumba"* inaunda taswira ya udhalilishaji na mateso ya kimwili na kisaikolojia, huku *"ulikula pesa kama ambazo zimekaangwa"* ikionyesha maisha ya anasa na upotovu. Picha hii inazua hisia za maumivu ya ndani, majuto makali na huzuni, hali inayomfanya mhusika ajitazame upya kwa mtazamo wa kujilaumu. Hali hii ndiyo inaunda kiini cha ujumi wa kimapenzi kwa kuonyesha mgongano wa hisia kati ya furaha ya anasa za awali na uchungu wa majuto baadaye. Sentensi hii inamwongoza msikilizaji kupitia hisia za majuto, huzuni na uhalisia wa maisha. Inaeleza jinsi mtu anavyoweza kuangamia kijamii na kifamilia kwa sababu ya matumizi mabaya ya fedha. Zaidi ya hayo, matumizi ya taswira ya "kupigwa mateke na watoto ukiwa umelala kwenye ferada mwa nyumba," yanamfanya msikilizaji atafakari hali ya mtu aliyetelekezwa, ambayo ina ladha ya uzuri wa huzuni. Pia kuna hisia za kupoteza utu, za mtu anayeanguka kutoka hali ya heshima hadi unyonge wa mwisho, jambo linaloibua hisia za huruma. Kwa hivyo, kupitia ujenzi wa sentensi ndefu yenye hisia nzito na picha inayochochea fikra za kina juu ya maisha na maadili, mwimbaji anadhihirisha wazi ujumi wa kimapenzi.

Katika muziki GF mwimbaji ametumia picha za vitu halisi kumleta msikiliziji katika ulimwengu wake wa kihisia. Kwa mfano taswira za umbali na safari zinajitokeza katika sentessi hizi;
*Nieendaa airport mbangite nyie ulisa ndeke* - Huwa ninaenda katika uwanja wa ndege nikiwa na mpango wa kuabiri ndege (ubeti wa tatu, mshororo wa kwanza)

*Ngesilya ivitha nilise meli Mombasa kuu* - Nafikiria kujificha niabiri meli huko Mombasa (ubeti wa nne, mshoror wa kwanza)

Sentensi hizi zinajenga taswira ya safari ya mwimbaji na vikwazo anazokabiliana nazo anapojitayarisha kumtembelea mpenzi wake. Vilevile safari ya mwimbaji kwenda Ujerumani inaonyesha taswira ya umbali wa kihisia uliopo baina yake na mpenzi wake. Mishororo hii inaonyesha ujumi wa kimapenzi kwa kuonyesha hisia za ndani za mwimbaji zinazomsukuma kufanya juhudi za kumtembelea mpenziwe.

**4.4 Ujumi wa Kitamaduni**

Ujumi wa kitamaduni unahusisha mikakati ya kisanaa inayoakisi na kuwasilisha maadili, utambulisho na tajriba za jamii fulani. Eagleton (1990) na Thiong'o (1986) wanasisitiza kuwa ujumi wa kitamaduni umefungamana kwa kina na itikadi pamoja na utambulisho wajamii. Katika muziki, ujumi wa kitamaduni huimarishwa kupitia matumizi ya lugha za asili, ala za kitamaduni, mitindo ya uigizaji na uimbaji pamoja na maudhui yanayoshabihiana na maadili ya kijamii na hali halisi ya maisha (Finnegan, 1970; Turino, 2000). Waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba wameimarisha ujumi huu kama ifuatavyo;

Katika muziki SY tazama sentensi zifuatazo;
*Ndinenenaa na andu mwanake, ndakyongete ni mutavye* - Huwa sizungumzi na watu mimi, kama sijatafuna miraa (ubeti wa nne mshororo wa kwanza)
*Matesi ni mundu vathei, Matenzawa ngesa utema* - Huwa hawajui mimi ni bure, Matenzawa nisipotafuna miraa (ubeti wa tatu mshororo wa tatu)

Ujumi wa kitamaduni unaojitokeza katika muziki huu unaeleweka kupitia matumizi ya lugha na maudhui yanayoakisi maisha halisi ya jamii ya mwimbaji. Sentensi hizi, zimetumia mkakati wa ukiushi ambao unavunja kanuni za kisarufi za lugha ya Kikamba, hasa kwa kuingiza neno la Kiswahili "miraa." Hili linaibua ujumi wa kitamaduni kwa sababu linaakisi matumizi ya lugha inayotokana na mwingiliano wa maisha ya kisasa na utamaduni asilia.

Mwimbaji ametumia neno *miraa* kama dhana inayotambulika kijamii ili kuonyesha tabia inayofungamana na utamaduni wa jamii yake. Miraa hapa sio mmea wa kawaida, bali ni kiwakilishi cha tabia, mienendo na mitazamo inayotambuliwa na jamii ya mwimbaji. Kwa hivyo, sentensi hizi zinadhihirisha namna mwimbaji anavyojitambulisha kama mshiriki halisi wa jamii yake, kueleza hali zake za kiakili, kijamii na kitamaduni kupitia matumizi ya neno "miraa" kama kitambulisho cha maisha yake ya kila siku. Kwa njia hii, muziki huu hauwasilishi tu ujumbe wa kibinafsi, bali unatoa nafasi ya msikilizaji kutambua na kuhusiana na mazingira ya kitamaduni ya mwimbaji. Ujumi huu unatoa taswira ya kijamii inayohusisha matumizi ya lugha mseto na tabia ya kijamii kama vile kutafuna miraa.

Katika muziki RN ujumi wa kitamaduni umeimarishwa kupitia matumizi ya mikakati ifuatayo;
*Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uya oou ta ngaange*- Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa (ubeti wa kwanza, mshororo wa kumi na mbili)

*Na wathelelwa mayosa abiria ungi, Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Na ukiishiwa wanachukua abiria mwingine, Unaachwa kwenye baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini (ubeti wa kwanza mshororo wa saba na nane)

Ujumi wa kitamaduni katika muziki huu umeimarishwa kupitia matumizi ya misemo isiyo ya kawaida, ya kejeli na yenye taswira ili kuvutia hisia na fikra za msikilizaji. Kauli kama, *"Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange"* na *"Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya"* ni mifano ya matumizi ya sitiari na lugha ya taswira inayochanganya uhalisia wa maisha ya kijamii na uzito wa kitamaduni. Misemo hii inavunja matumizi ya lugha ya moja kwa moja kwa kutumia lugha ya picha na kejeli ambayo inahusishwa na maisha ya kawaida ya jamii ya Wakamba. Kwa mfano, tashbihi ya "kutumia pesa kama ambazo zimekaangwa" inawasilisha dhana ya ubadhirifu kwa njia ya kuchekesha lakini yenye ujumbe mzito ilhali "kuachwa kwa baridi kama mtoto wa maskini" inasisitiza hatari ya kutokuwa na mipango au uangalifu wa kifedha. Mikakati hii imetumika kuimarisha ujumi wa kitamaduni kwa kuonyesha maisha halisi, tabia na changamoto zinazokumba vijana na wanajamii kwa ujumla. Kwa hivyo, ujumi huu unafanya muziki huu kuwa sio tu kwa ajili ya burudani, bali pia chombo cha mafunzo, maonyo ya kijamii na uhifadhi wa utamaduni wa jamii. Matokeo haya yanalingana na madai ya Barber (1987), kwamba lugha ya kisanii inayotumika katika muziki huchanganya burudani na mafundisho ya kijamii ili kuufanya muziki kuwa chombo madhubuti cha kufundisha, kuonya na kuendeleza utamaduni.

Vilevile katika muziki RN mishororo ifuatayo inaakisi ujumi wa kitamaduni;
*Raha Ndukauna Kuma Tene Ndukauna, Tindikana nawo indi mwiso ukaiya* - Raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii, Sukumana nayo lakini mwisho utalia. (ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza)

Mishororo "raha haitawahi saidia, kutoka zamani raha haisaidii, sukumana nayo lakini mwisho utalia" unaakisi maadili ya jamii ya Wakamba kuhusu umuhimu wa kujizuia, kuwajibika na kutafakari athari za matendo ya muda mfupi. Hapa, ujumi huu wa kitamaduni umejengwa kupitia ukinzani kati ya raha ya muda mfupi na mateso ya baadaye. Hali hii inaibua falsafa ya maisha inayosisitiza busara, nidhamu na

utunzaji wa rasilimali kwa mustakabali bora. Matokeo haya yanaonyesha namna muziki unavyotumika kama chombo cha kuendeleza na kueneza maadili ya kijamii, hasa yale yanayohimiza uwajibikaji. Kwa hivyo, muziki huu hauwasilishi tu ujumbe wa kihisia bali umebeba maadili ya kijadi yanayowiana na mitazamo ya jamii kuhusu maisha bora na yenye heshima. Matokeo haya yanakubaliana na hoja ya Thiong'o (1986) anayesisitiza kuwa kazi za kisanaa zinapaswa kufungamana na maisha ya jamii na kuwa sehemu ya mchakato wa jamii kwa kuendeleza maadili na uelewa wa hali halisi. Aidha, Finnegan (1970) anaeleza kuwa wasnii katika fasihi simulizi, wakiwemo waimbaji na washairi wa jamii za Kiafrika, hutumia lugha ya kinathari na ushairi kuhamasisha tabia njema, nidhamu na kuonya dhidi ya matendo yanayoweza kuhatarisha maisha ya mtu au jamii.

Kwa hivyo, kama inavyobainishwa na watafiti hawa, muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba unatumika kama chombo cha mafunzo ya kijamii na utamaduni. Ujumi wa kitamaduni katika muziki huu unahimiza maadili kama vile uwajibikaji, heshima na maisha yenye mwelekeo wa kiutu.

**4.5 Ujumi wa Kiishara**

Ujumi wa kiishara katika muziki unahusisha matumizi ya lugha ya ishara na sitiari ili kuibua hisia badala ya kupitisha ujumbe kwa njia ya moja kwa moja au ya wazi. Mtindo huu humwezesha msikilizaji kupata maana kupitia taswira za kisanaa, toni ya sauti na tamathali za usemi kama zinavyotumika katika tungo. Kama wanavyoeleza Balakian (1967), Fisher (2015) na Hatten (2018), hali ya utata na kutoeleza jambo moja kwa moja, ni kiini cha ujumi huu. Jambo hili huwezesha msikilizaji kushiriki kihisia kwa undani zaidi. Kama anavyoeleza Finnegan (1970), matumizi ya lugha ya ishara katika kazi za fasihi ya Kiafrika kama vile sitiari na methali huwezesha kupitisha maana tata za kijamii. Katika muziki wa Benga ujumi wa kiishara umeimarishwa kupitia mitindo mbalimbali. Kwa mfano; Katika muziki RN mwimbaji ametumia sentensi zifuatazo za kisitiari na tashbihi;

"*Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki* - Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana" (ubeti wa kwanza mshororo wa kumi na mbili)
"*Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya* - Unaachwa kwa baridi na kuteseka kama mtoto wa maskini" (ubeti wa kwanza mshororo wa nane)

Katika mishororo hii, ujumi wa kiishara unajitokeza kupitia matumizi ya sitiari na tashbihi, ambazo zimetumika kuibua hisia na kuchochea tafakari za msikilizaji badala ya kueleza maana kwa njia ya moja kwa moja. Mshororo *"Ivundisye kusuvia mbesa syaku mwanake na uiyeka uyaa oou ta ngaange, ti mboneki-* Jifunze kutunza pesa zako kijana, na uache kuzitumia hivyo kama ambazo zimekaangwa, si rahisi kupatikana*"* unalinganisha ubadhirifu wa pesa na kuzitumia kama chakula kilichokaangwa, tamathali inayojenga picha yenye nguvu kuhusu matumizi ya fedha yasiyo ya busara. Hii ni sitiari yenye uzito wa kihisia inayosababisha msikilizaji afikirie kwa kina kuhusu madhara ya kifedha. Vilevile, katika mshororo *"Uilekelwa mbevo uithina ta kana ka ngya"*, tashbihi ya kuteseka kama mtoto wa maskini inaibua huruma na huzuni, ikionyesha matokeo ya kuishi bila kuwajibika kifedha. Matokeo haya yanaakisi maoni ya Grensideng na wenzake (2023) wanaoeleza kuwa lugha ya kitamathali katika nyimbo huunda picha za kudumu katika akili za wasikilizaji na kuchochea mwitikio wa kihisia. Vilevile, Leech (1969) anasisitiza kuwa lugha ya ishara hutumika na waimbaji kuibua hisia, kuongeza mvuto wa kisanaa na kufikisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kiini cha ujumi wa kiishara ni kutumia lugha ya picha na ishara ili kufikisha maana fiche, kuamsha hisia na kuhimiza tafakari za kina. Kwa hivyo ujumi wa kiishara katika muziki huu unahimiza uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali kwa njia inayovutia wasikilizaji.

Pia, katika muziki WM;
*Unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* – Unatumia pesa zangu bila aibu (ubeti wa kwanza mshororo wa tatu)
*Uwasa uu wonyoonyaa ndienda kisinga* - Urafiki huu wa kuninyonya sitaki Kisinga (ubeti wa nne mshororo wa nne)

*Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama...na ndwi thoni nakuivia nginya leu wa utuku- huwa* - Nawasaidia wanawake wako bila kuhisi gharama…. na hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi chakula cha usiku (ubeti wa tatu mshororo wa kwanza na wa tatu)

*Twataanisya uilika tulavu Mukuru, Uyambiiya uzambasya uivoya kimee* – Tukiachana unaingia vilabu vya Mukuru, unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe (ubeti wa nne mshororo wa kwanza na wa pili)

Katika muziki huu, ishara mbalimbali zimejengewa ndani ya lugha ya maumivu, kejeli na unyonyaji ili kufikisha ujumbe kuhusu urafiki wa kijamii unaolenga maslahi ya upande mmoja. Kauli kama: *"unyonyae tupesa twakwa uteiwa nthoni* - Unatumia pesa zangu bila aibu na *Uwasa uu wonyoonyaa ndienda kisinga* - Urafiki huu wa kuninyonya sitaki Kisinga," zinafichua dhana ya unyonyaji na usaliti lakini si kwa njia ya lawama ya moja kwa moja, bali kupitia mfumo wa picha na kinaya. Pia, kauli kama "*Nisuvia iveti syaku ndeiwa ngalama, na ndwi thoni nakuivia nginya leu wa utuku* - Nawasaidia wanawake wako bila kuhisi gharama, na hauna aibu nilikuwa nakulipia hadi chakula cha usiku" zinaonyesha ishara ya gharama kama picha ya mzigo wa kihisia na kifedha alionao mwimbaji. Hili linaashiria mgongano wa matarajio na uhalisia ambapo mwimbaji amechoshwa na mahusiano ya upande mmoja. Aidha, taswira ya mwimbaji kuwafadhili wanawake wa

rafiki yake kwa kuwanunulia pombe na chakula, ni ishara ya unyonge na imetumika kisitiari kuonyesha jinsi mwimbiji anavyonyanyaswa bila shukrani. Kauli "Twataanisya *uilika tulavu Mukuru uyambiiya uzambasya uivoya kimee* - Tukiachana unaingia vilabu vya Mukuru unaanza kunidhalilisha ukiomba pombe," inaonyesha namna jina la mwimbaji linavyopakwa tope katika maeneo ya vileo. Jambo hili ni ishara ya fedheha na usaliti wa urafiki. Ujumi wa kiishara katika muziki huu umejengwa kupitia lugha ya picha, sitiari na urudiaji wa maudhui ili kuwasilisha ujumbe wa kuchoshwa na mahusiano ya kirafiki yasiyo na usawa. Msanii anawakilisha hisia za kuchoshwa, kuumizwa na kuamua kuvunja urafiki kwa njia inayoibua hisia za kutafakari na kuelewa undani wa mateso ya urafiki huo. Hivyo basi, muziki huu umetumia ujumi wa kiishara kuwasilisha uzoefu wa kibinafsi kwa njia inayovutia na kutoa nafasi ya ufasiri mpana wa kijamii.

**4.3.6 Ujumi wa Kisiasa**

Ujumi wa kisiasa hurejelea namna kazi za kisanaa hutumia mbinu za kitamathali kama vile, sitiari, tashbihi na taswira kuwasilisha mijadala ya kisiasa, maoni ya kijamii, au msimamo wa kisiasa, kwa njia ya kiubunifu inayovutia hadhira na kuibua tafakari. Kwa mujibu wa Rancière (2004), ujumi wa kisiasa ni njia ya kusawiri au kupinga mamlaka, ukandamizaji, au ahadi za uongo kupitia mbinu za kisanii. Muziki, kama anavyobainisha Street (2013), ni jukwaa la kipekee la kueleza maumivu, matarajio na usaliti wa kisiasa kwa njia ya hisia na lugha ya sanaa. Ujumi huu umeimarishwa katika muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba kama ifuatavyo;

Katika muziki wa Benga, ujumi wa kisiasa umebainika kupitia matumizi ya maswali ya balagha, lugha ya hisia, sitiari na urudiaji, unaowasilisha hali ya kukatishwa tamaa na usaliti wa kisiasa. Kwa mfano katika mshororo huu;

*Ninguseng'a na ngikulya ii munene we kowolilwe* - Ninashangaa na kuuliza, mkubwa kwani ulisahau? (kibwagizo cha muziki MK)

Mshororo huu unaorudiwa mwishoni mwa kila ubeti unadhihirisha masikitiko ya wananchi waliojitolea katika kampeni kwa matumaini ya kuboresha hali yao, lakini walipata kutelekezwa baada ya kiongozi kupata mamlaka.

Vilevile katika muziki huu MK mishororo ifutayo:
*Kivila niwoosie na nyie ndwanzuvia* - Kiti ulichukua na mimi haunitunzi (ubeti wa kwanza mshororo wa tano)
*Navoyaa ngai mwa autetheye* - Nilimwomba mungu angalau akusaidie (ubeti wa pili mshororo wa kwanza)
*Unene ni twosie nanotukuthinaa* - Tuliuchukua lakini bado tuko na shida (ubeti wa pili mshororo wa sita)
*Ningutulya ndu na kwita uekeo* - Ninapiga magoti na kuomba (ubeti wa tatu mshororo wa kwanza)

Mishororo hii inatilia mkazo usaliti wa kisiasa, ambapo mwananchi ananyimwa matunda ya ushindi alioupigania. Ubeti wa pili unadokeza wazi hali ya imani na matumaini: "Nilimwomba naomba Mungu angalau akusaidie... lakini bado tuko na shida", kauli hii inaonyesha namna siasa zinavyotumika kama chombo cha matumaini ya mabadiliko, lakini baadaye matumaini haya yanageuka kuwa chimbuko la maumivu. Katika ubeti wa tatu, kwa kutumia lugha ya unyenyekevu kama *"napiga magoti na kuomba msamaha"*, unaibua picha ya mnyonge anayeomba rehema mbele ya kiongozi aliyemtelekeza, hali inayoonyesha mgawanyiko wa nguvu za kijamii kati ya viongozi na wananchi.

Ujumi wa kisiasa katika muziki huu umeimarishwa kupitia matumizi ya lugha ya maumivu na kejeli ili kuwasilisha mivutano ya mamlaka, hali ya kupuuzwa kwa wananchi na usaliti wa kisiasa. Muziki huu hauwasilishi tu hisia za msanii, bali ni sauti ya walio wengi na waliokatishwa tamaa. Matokeo haya yanaendana na hoja ya Street (2013) kuwa muziki una uwezo wa kipekee wa kuunganisha hisia za binafsi, hali za kisiasa na kuibua hoja nzito kwa njia ya kisanaa.

## 5.0 HITIMISHO

Utafiti ulibainisha kuwa waimbaji wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba hutumia mikakati mbalimbali ya kimtindo kama nyenzo ya kuimarisha ujumi. Mikakati hii hujitokeza katika matumizi ya tamathali za usemi, mbinu za kisemantiki, mitindo ya kisintaksia na uundaji wa taswira za kisanaa ambazo huakisi mitazamo ya ujumi wa kigothiki, kihalisia, kimapenzi, kisiasa, kitamaduni na kiishara. Kupitia aina hizi za ujumi, waimbaji huweza kuwasilisha hisia za huzuni, mapenzi, usaliti, matumaini na hata ukosoaji wa kijamii na kisiasa kwa njia ya kisanaa yenye mvuto na athari za kudumu kwa hadhira.

Matokeo yanaonyesha kwamba umuhimu wa muziki wa Benga wa jamii ya Wakamba si tu burudani, bali ni chombo cha mawasiliano chenye uzito wa kijamii na kisanaa. Mikakati ya kimtindo inayotumiwa huchangia katika kudumisha lugha na utamaduni wa jamii ya Wakamba, kutoa fasiri mbadala za maisha halisi na kuimarisha ushiriki wa hadhira kwa kuwahusisha kihisia na kiakili. Kwa hivyo, uchanganuzi wa ujumi katika muziki huu unatoa mchango muhimu kwa taaluma ya isimu na fasihi na kuchangia uhifadhi wa urithi wa lugha na utamaduni wa Kiafrika kwa jumla.

## MAREJELEO


- Abrams, M. H. (1999). A Glossary of Literary Terms, Seven Edition. *Cornell University Heinle & Heinle Thomson Learning*.
- Afipah, E., & Andriani, Z. Z. D. (2022). Critical Discourse Analysis of Lonely Song Lyrics by Justin Bieber. Darussalam English Journal (DEJ), 2(1), 99-127.
- Anudo, C. N. A., & Awuor, Q. E. (2018). Music the loaded weapon: War metaphors & ethnicity in

Kenyan songs. *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa, 9(1), 29-68.*

- Balakian, A. (1967). *The Symbolist Movement: A Critical Appraisal*. New York: Random House.
- Barber, K. (1997). *Readings in African Popular Culture*. Oxford: James Currey.
- Bitababaje, H. W. Hali ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa: mfano nyimbo za Christina Shusho (Doctoral dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma).
- Bradley, S. (2018). *Gothic soundscapes in modern music*. Bloomsbury Academic
- Butler, P. G. (2004). *Out of style: A retrospective and prospective look at style in composition theory and practice*. Syracuse University.
- Byron, G., & Townshend, D. (Eds.). (2014). *The Gothic World* (pp. 1764-1850). London: Routledge.
- Doyle, S. (2013). A review of Millie Taylor's musical theater, entertainment and realism. *Critical Voices: The University of Guelph Book Review Project*, *3*(3), 22-30.
- Eagleton, T. (2008). *Literary theory: An introduction* (2nd ed.). University of Minnesota Press.
- Enon, J. C. (1998). Educational research, statistics and measurement. *Kampala: Makerere University*.
- Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa*. Oxford University Press.
- Fisher, R. (2015). *Symbolism and Music: The Unspoken Meaning*. *Journal of Aesthetic Education*, 49(3), 23–38.
- Fitzgerald, S. (2010). *Romanticism and the sublime: The social nature of aesthetics*. Cambridge University Press.
- Grensideng, W., & Agung, I. G. A. M. (2023). Analysis of Figurative Language in Stephen Sanchez's Song Lyrics. *Journal of English Language Teaching and Literature (JELTL)*, *6*(1), 27-39.
- Hatten, R. (2018). *A Theory of Virtual Agency for Western Art Music*. Indiana University Press.
- Kant, I. (2000). *Critique of the power of judgment* (P. Guyer & E. Matthews, Trans.). Cambridge University Press.
- Kenyan History Team. (2025, January 2). *The rhythm of Kenya: How youth drive the evolution of popular music*. Kenyan History.
- Kithome, C. K. (2012). *Vernacular radio and traditional music practices in Kenya: case study: Kamba radio of the Kamba community* (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).
- Kombo, D. K na Tromp, D.L. A (2006). Proposal and Thesis Writing: An introduction. Nairobi: Pauline Publications Africa.
- Kothari, C. (2017). research methodology methods and techniques by CR Kothari. *Published by New Age International (P) Ltd., Publishers*, *91*.
- Laswai, A. (2015). Laswai, A. Ujumi katika muziki wa dansi: mfano kutoka nyimbo teule za Marijani Rajabu na Ally Choki (Doctoral dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma).
- Leech, G. N. (1969). A Linguistic Guide to English Poetry *(English Language Series)*. Perason Professional Education*,* USA: Longman Publishers
- Menninghaus, W., Wagner, V., Wassiliwizky, E., Knoop, C. A., & Jacobs, A. M. (2022). Parallelisms and deviations: Two fundamentals of an aesthetics of poetic diction. *Philosophical Transactions of the Royal Society B: Biological Sciences, 377*(1841), 20200389. https://doi.org/10.1098/rstb.2020.0389
- Muema, A. K. (2019). *The Linguistic Devices of Euphemism in Kamba: a Case of Kamba Benga Music* (Doctoral dissertation, University of Nairobi). http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/109445
- Mutisya, B. M., & Muhoro, P. (2022). Aesthetic Values in Kamba Children's Play Songs.
- Okal, B. O. (2020). A Psycho-Realist Analysis of Gabriel Omolo's' Lunch Time'Music. *EAS Journal of Humanities and Cultural Studies July*. https://doi.org/10.36349/EASJHCS.2020.V02I04.03
- Rancière, J. (2004). *The Politics of Aesthetics: The Distribution of the Sensible*. London: Continuum.
- Scruton, R. (1997). *The aesthetics of music*. Oxford: Oxford University Press.
- Spooner, C., & McEvoy, E. (Eds.). (2007). *The Routledge companion to gothic* (p. 38). London: Routledge.
- Street, J. (2013). *Music and politics*. John Wiley & Sons.
- Tagg, P. (2012). *Music's meanings: A modern musicology for non-musos*. New York
- Thiong'o, K. J., Wanjiku, K., & Kimingichi, W. (2022). Stylistic choices in three Bongo Flava songs: "Rita", "Pii Pii" by Marlaw, and "Nikifa Kesho" by Diamond Platnumz. *Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies*, *1*(1), 33-54.
- Turino, T. (2000). *Nationalists, Cosmopolitans, and Popular Music in Zimbabwe*. University of Chicago Press.

**Cite This Article:** Carolyne Muthini Mutuku, John Khaisie Wanyama, Timothy Kinoti M'ngaruthi (2025). Uchambuzi wa Ujumi katika Muziki wa Benga wa Jamii ya Wakamba: Mkabala wa Umtindo. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 8*(9), 503-512.